

# CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI

## WITO WA MAKALA/CALL FOR PAPERS 2018

*Kiswahili, Kioo cha Lugha na Mulika* ni Majarida yanayochapishwa na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Majarida yote matatu ni ya kitaaluma na huchapishwa mara moja kwa mwaka.

TATAKI inapenda kuwatangazia wadau mbalimbali kwamba inapokea makala kwa ajili ya majarida yake kwa matoleo ya mwaka 2018 kwa ajili ya kufikiriwa kuchapishwa. Tunakaribisha makala yanayohusu Fasihi au Isimu ya Lugha ya Kiswahili, utamaduni na mengine yenye mrengo huo.

### **Mtindo wa Makala:**

1. Makala yapigwe chapa kwenye karatasi za A4.
2. Makala yawe na: Kichwa cha habari (Mada), Jina la mwandishi/waandishi, anuani ya barua pepe na asasi au Chuo Kikuu atokacho mwandishi (pale inapobidi)
3. Makala yawe yameambatana na ikisiri fupi inayoeleweka na yenye urefu wa maneno 150-250. Ikisiri iwe mwanzoni mwa makala chini ya taarifa zilizotajwa hapo juu.
4. Makala yawe yamechapwa kwa kutumia programu ya *Word* na kukiwa na nafasi 1.5 kati ya mstari na mstari.
5. Makala yawe na urefu kati ya maneno 4000-7500.
6. Mapitio ya vitabu (Book Review) yawe na maneno kati ya 800-1200.
7. Tanbihi zote ziwekewe namba na zitumike pale tu inapobidi.
8. Marejeo yapangwe kialfabeti, majina ya vitabu yaandikwe kwa italiki.

### **Marejeo (kwa mfano)**

Mulokozi, M.M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mekacha, R.D.K. (1997). 'Disconnecting Education,' katika *Journal of Linguistics and Language in Education*, 3: 95-105. Dar es Salaam: Idara ya Lugha ya Kiswahili na Isimu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

**TANBIHI:** Tunapenda kusesitiza kuwa kabla mwandishi hajatuma makala yake, ayapitie kwanza na kujiridhisha kuwa makosa yote yamerekebishwa kwa kiwango chake. Pia, tunaweka msisitizo katika kufuata taratibu za majarida yetu ikiwa ni pamoja na kuandika kwa mtindo wa makala na si ripoti ya utafiti. Kama makala hayatakuwa yamefuata taratibu na kuhaririwa vizuri na mwandishi, hatutayashughulikia.

Zaidi ya hayo, tunasisitiza kuwa makala yatumwe kwenye Jarida moja kati ya hayo matatu na siyo kutuma makala moja kwenye jarida zaidi ya moja. Tuma makala yako kabla ya *Send your paper before* **Septemba 15, 2017**. Kwa maelezo zaidi wasiliana na wahariri wanaohusika *For more information contact the respective editors*.

**TUMA MAKALA YAKO KWA/SEND YOUR PAPER(S) TO:**

***KISWAHILI JOURNAL*** (Makala yaandikwe kwa Kiswahili au Kiingereza)

WAHARIRI/EDITORS

Prof. D.P.B. Massamba      massamba45@gmail.com  
Mr. Festo Joster              josterfesto@yahoo.com

***MULIKA JOURNAL*** (Makala yaandikwe kwa Kiswahili tu)

WAHARIRI/EDITORS

Prof. M.M. Mulokozi      tamulokozi50@yahoo.co.uk  
Dr. Mussa Hans              mussahans30@gmail.com

***KIOO CHA LUGHA JOURNAL*** (Makala yaandikwe kwa Kiswahili au Kiingereza)

WAHARIRI/EDITORS

Dr. Shani Omari              shaniom@yahoo.co.uk  
Dr. Rhoda Peterson          kidamis@yahoo.com